

Nelson Mandela (Rais wa kwanza mzale

MWANANCHI UK 10

# *Bima ya mifugo isiishie mijini tu *

Moja kati ya habari zilizokuwemo kwenye gazeti hili toleo la jana ni kuzinduliwa kwa 'Bima ya Mifugo' nchini, ambayo inaeleza itatoa ulinzi na kupunguza maumivu anayoyapata mfugaji yanapotokea majanga mbalimbali.

Wizi wa mifugo, magonjwa na mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha ukame wa mara kwa mara ni kilio cha muda mrefu sasa, wafugaji wamekuwa wanapoteza mifugo yao na kupoteza ukwsi wao bila kuwepo wa kuwafidia.

Katikati ya mtanziko huo, bima hiyo mpya ijulikanayo kama Index-Based Livestock Insurance (IBLI) imezinduliwa mwishoni mwa wiki na kampuni ya ACRE Africa kwa kushirikiana na Phoenix of Tanzania Assurance.

Katika mazingira tuliyonayo ambayo tumeyaeleza hapo juu ni muhimu kundi hili la uzalishaji liingia kwenye bima kwa kuwa itasaidia kupunguza vilio vya kupoteza mifugo.

Ni imani yetu kwamba masharti ya kuingia kwenye huduma hii yatakuwa rafiki na kuwavutia watu wengi ambao awali walikuwa wanapata hasara kubwa za mara kwa mara.

Hata hivyo, tunadhani ili kufanikisha malengo ya kipla upande, ni vizuri elimu ya kina ikatolewa katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwashirikisha viongozi kuanzia ngazi za chini na wafugaji wenyewe, ili kila mmoja si tu aelewe faida zake bali pia waitumie bima hiyo kwa faida yao.

Licha ya umuhimu wa huduma hii, si ajabu ikaishia mjini kama tunavyoziona nyingine, ndiyo maana tunashauri iangalie pia vijijini ambako kuna wahitaji wengi na ndiko mara kwa mara yanapotekea majanga yahusishayo mifugo kama mapigano kati ya wafugaji na wakulima, ukame na mengineyo.

Ni ukweli usiopingika kuwa huduma nyingine huanzishwa mijini kutokana na sababu ya ubora wa miundombinu, urahisi wa kuwafikia walengwa, uelewa wa watu husika na uwezo wa kuchangia, hata hivyo wakazi wa vijijini wakati mwingine ndiyo wahitaji zaidi wa huduma husika.

Tunaposhuhudia mapigano kati ya wakulima na wafugaji si kwamba wanapenda kufanya vurugu, bali hakuna uwekezaji wa kusaidia shughuli za kundi moja kufanyika pasi kuathiri kundi jingine.

Tunapozungumzia ufugaji au kilimo cha kisasa ni lazima tutenge maeneo ya shughuli hizo na kuwawezesha wahusika.

Leo hii wafugaji wanaingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kusaka malisho ilhali mkulima anategemea kilimo kwa ajili ya chakula na biashara kukidhi mahitaji ya kila siku.

Kama wafugaji watakuwa na uhakika wa bima ya mifugo yao, wanaweza pia kumudu gharama za kulipa inapotokea mifugo yao kula mazao ya wakulima, kutegemeana na masharti ya bima husika.

Tunaamini bima za aina hii zinapaswa ziende mbalimbali zaidi katika makundi mbalimbali kwenye jamii kuepusha umasikini wanaoupata watu pale mali zao zinapoathirika kwa namna yoyote ile.

Hatutarajii kusikia vikwazo vya kufika maeneo ya vijijini ninakwamisha bima hii, bali tungependa kusikia wadau wanaotoa huduma wakishirikiana ama na Serikali au washirika wengine kufikia malengo ya kibiashara na utoaji huduma.

Ni dhahiri shahiri suala hili ni la muhimu na hivyo bima ya mifugo iungwe mkono kwa manufaa ya kundi hili. Ufugaji wa kisasa uwe sehemu ya mapinduzi ili kila upande uweze kuona tija na hatimaye kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi na mtu mmojammoja.

CamScanner

Kwa mujibu wa taarifa kutoka nchini humo, tetemeko hilo pia liliathiri pwani

Michel-Olivier, alinukuliwa akisema wana changamoto kubwa ya shughuli za

kipimo cha richa 6.7, ilisababisha vifo vya watu 12,000 katika mji wa Agadir, nchini humo.

UHURU UK 22.

# Misri kufanya uwekezaji biashara ya nyama Tanzania




**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia) akitoa ufafanuzi kwa Waziri wa Kilimo kutoka nchini Misri, El Sayed El Kosayer kuhusu fursa zilizopo katika sekta za mifugo na uvuvi walipokutana jijini Dar es Salaam.**

**Na MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekutana na kuzungumza na Waziri wa Kilimo kutoka nchini Misri, El Sayed El Kosayer, ili kuona uwezekano na kuweka mazingira wezeshi ya biashara hiyo baina ya nchi hizo mbili.

Waziri Ulega alifanya mazungumzo hayo na El Kosayer kando ya Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Pamoja na kujadiliana mambo mengine, suala la biashara ya nyama kutoka Tanzania kwenda kuuzwa nchini Misri lilijadiliwa kwa kina huku El Kosayer akiahidi kulifanyia kazi kwa haraka ili biashara hiyo iweze kuleta matunda kwa pande zote mbili.

Mapema wakati wa mazungumzo yao, Kosayer alimweleza Waziri Ulega kuwa lengo la kukutana kwao ni kuona namna wanavyoweza kuendelea kuimarisha ushirikiano katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi ili ziweze kuwanufaisha wananchi wa pande zote mbili.

UHURU UK 16.

TAHADHARI>> Wana

# Ulega ateta na kigogo wa FAO

**Na MWANDISHI WETU**

SHIRIKA la Kimataifa la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), limesema litaendelea kushirikiana na Tanzania kuendeleza sekta za mifugo, uvuvi na kilimo, kuwawezesha wanawake kushiriki shughuli za uzalishaji mali.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika Afrika, Abebe Haule-Gabriel, alipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula barani Afrika (AGRF), jijini Dar es Salaam.

"Waziri ninaomba kutumia fursa hii kukueleza FAO tumekuwa na ushirikiano mzuri na Tanzania, tutaendelea kushirikiana kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kuendelea kuwainua wanawake na vijana," alisema.

Kwa upande wake, Ulega aliishukuru FAO kwa ushirikiano wa kifedha na kitaalamu wanaoutoa katika miradi mbalimbali inayolenga kusimamia na kuendeleza rasilimali ya uvuvi hususan utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa Uvuvi Mdogo (SSF Guidelines).

Waziri huyo alisema mambo mengi ambayo FAO inashirikiana na Tanzania ni Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi na kuwawezesha wanawake katika sekta ya uvuvi na Serikali ipo tayari kuendelea kushirikiana na shirika hilo.

**Uvuvi**

## USHIRIKIANO

FAO tuna ushirikiano mzuri na Tanzania na tutaendelea kushirikiana kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi

hivyo maji yanaweza kurudia njia nyingine na kusababisha maafa na

za binadamu zikiongezeka.

kunyesha katika mikoa mbalimbali nchini.

## MAZUNGUMZO

UHURU





**WAZIRI** wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akizungumza na Mkurugenzi Msaidizi na Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) Afrika, Abebe Haule-Gabriel, wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AGRF), uliomalizika hivi karibuni, Dar es Salaam. (Na Mpigapicha Wetu).

CamScanner

THE GUARDIAN Page 20.





Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega (Front row, L) is pictured playing the drum at the closing of livestock system forum held in Dar es Salaam last weekend. PHOTO: CORRESPONDENT JUMANNE JUMA